optima

# **Matukio ya Kufungwa kwa Huduma ya Intaneti Nchini Tanzania:** Ukadiriaji wa Mahitaji na Uwezo wa Kujiandaa, Kuzuia, Kupinga




## Kuhusu Ripoti Hii

Tangu 2019, mradi wa OPTIMA wa shirika la Internews umekuwa ukishirikiana na mashirika ya asasi za kiraia katika nchi mbalimbali duniani ili kujiandaa vyema, kuzuia na kupinga matukio ya kufungwa kwa huduma ya intaneti. Mwaka wa 2022, shirika la Internews lilishirikiana kwa ukaribu na mashirika kama vile TAMWA, Zaina Foundation na Change Tanzania, ili kushiriki katika mchakato wa kina wa ukadiriaji wa mahitaji ili kuelewa uwezo wa asasi za kiraia nchini Tanzania wa kushiriki katika harakati za kupinga matukio ya kufungwa kwa huduma ya intaneti.

Kupitia utafiti wa wadau wa asasi za kiraia pamoja na mfululizo wa mazungumzo ya makundi lengwa kama sehemu ya warsha iliyobuniwa kwa pamoja, ripoti hii inachunguza jinsi asasi za kiraia nchini Tanzania zinavyochukulia changamoto za harakati za utetezi kuhusu matukio ya kufungwa kwa huduma intaneti, mitazamo kuhusu uwezekano wa kufungwa kwa huduma ya intaneti siku za usoni, na nyenzo zinazohitajika ili kujiandaa vyema na kuzuia matukio ya kufungwa kwa huduma ya intaneti.

Ripoti kamili, inayopatikana katika **preparepreventresist.org**, inatoa uchanganuzi wa kina wa kisheria pamoja na ukaguzi wa kina wa matokeo ya utafiti, na mazungumzo ya kundi lengwa. Ripoti inakamilika kwa kutoa mapendekezo kwa wadau wa asasi za kiraia, watunzi wa sera na mashirika ya kimataifa kuunga mkono uwezo wa wadau nchini Tanzania wa kukuza harakati za utetezi thabiti wa kudumu ili kuzuia matukio ya kufungwa kwa huduma ya intaneti.



## Muhtasari Mkuu

Wakati Naibu Rais Samia Suluhu Hassan alipochukua nafasi ya urais mnamo Machi 2021 baada ya kifo cha Rais John Magufuli, wawakilishi wa asasi za kiraia walisema kuwa "wana matumaini kwa tahadhari" kuhusu matarajio ya mabadiliko mazuri ya kidemokrasia. Uongozi wa kiimla wa miaka mitano wa hayati rais Magufuli ulikuwa umejumuisha kupitishwa kwa mkusanyiko wa sheria za kikatili zinazodhibiti uhuru wa raia na vyombo vya habari. Mtindo huo ulifikia upeo wa juu siku moja kabla ya uchaguzi wa Oktoba 2020, wakati nchi ilishuhudia tukio la kwanza la kufungwa kwa huduma ya intaneti. Huduma za Whatsapp, Facebook Messenger, Telegram na Twitter zilizuia, na ziliendelea kuzuiwa kwa kipindi chote cha uchaguzi, kwa angalau siku 11 (Viungo vya data ya OONI WhatsApp, Facebook Messenger na Telegram). Lakini miezi kadhaa tu baadaye, katika moja ya hotuba zake za kwanza, Rais Hassan alisema kuwa vyombo vya habari vinapaswa kufunguliwa tena, na alipuuzilia mbali dhana ya "kufifia kwa uhuru wa vyombo vya habari" nchini Tanzania.

Kumekuwa na baadhi ya ishara za kutia moyo, ikijumuisha kuondolewa kwa marufuku yaliyowekwa dhidi ya magazeti manne na taarifa rasmi za mara kwa mara zinazoahidi kufanywa kwa marekebisho ya Sheria ya Huduma za Vyombo vya Habari ya 2016 (2016 Media Services Act). Licha ya vitendo hivi vidogo na mazungumzo balagha ya awali, hakuna sheria yoyote kuu iliyopitishwa chini ya hayati raisi Magufuli (ikijumuisha Sheria ya Uhalifu wa Mtandaoni (Cybercrimes Act), Sheria ya Huduma za Vyombo vya Habari (Media Services Act), na Sheria ya Mawasiliano ya Kielektroniki na Posta ( Electronic and Postal Communications Act)) iliyorekebishwa wala kubatilishwa. Waandishi wa habari na wanaharakati wamendelea kukamatwa kwa makosa ya kukashifu, kuiga na kuchapisha habari za uongo chini ya Sheria ya Uhalifu wa Mtandaoni (Cybercrimes Act). Shirika la asasi za kiraia la Change Tanzania lilitueleza kwenye mchakato wa utafiti huu kwamba kuna pia "uhusiano wa karibu kati ya faragha na udhibiti nchini Tanzania," kwa sababu serikali hutumia Sheria ya Uhalifu wa Mtandaoni (Cybercrimes Act) kufikia mawasiliano ya faragha ya wanasiasa wakuu na waandishi wa habari, hatua inayosababisha hali ya hofu na kujidhibiti. Chombo fulani cha habari cha mtandaoni kilizuiwa kusasisha leseni yake baada ya kuripoti maandamano mwezi wa Julai 2022. Kamamwanaharakati mmoja alivyosema, "vyombo vya habari na waandishi wa habari wameondolewa "gerezani" kimfano tu, lakini sheria zilizowatia gerezani bado zipo."

Kutokana na kukwama katika hali hii ya hatihati ya kidemokrasia, asasi za kiraia nchini Tanzania zinakabiliwa na changamoto kubwa katika juhudi zake za kuleta mabadiliko muhimu na ya kudumu ya sera. Hata hivyo, fursa zinaweza kujitokeza, ikiwa, baada ya miaka ya kujidhibiti na hofu ya kulipizwa kisasi, serikali ya Rais Hassan itakubali hata kwa kiwango kidogo zaidi asasi za kiraia kufanya kazi kwa uwazi na kushirikisha serikali katika masuala ya uhuru wa vyombo vya habari na intaneti.

Huu ndio muktadha wetu wa utafiti huu ili kuelewa vizuri, katika kipindi hiki cha mabadiliko na shaka, kinachoweza kufanywa ili asasi za kiraia nchini Tanzania ziweze kujiandaa na kutarajia matukio ya kufungwa kwa huduma ya intaneti siku zijazo na kushiriki katika harakati za utetezi wa kudumu na kujenga muungano ili kuzuia matukio ya kudhibitiwa na kufungwa kwa huduma ya intaneti siku zijazo. Kulingana na wataalamu na watetezi walioshiriki kwenye utafiti huu, viongozi wa serikali hawajakubali tukio la

kufungwa kwa huduma ya intaneti la mwaka wa 2020 wala kuonyesha masikitiko yoyote au nia ya kuepuka mbinu hizo kuhusiana na chaguzi za miaka ijayo. Uchaguzi wa kimaeneo na uchaguzi mkuu unapofanyika mwaka wa 2024 na 2025, huu ndio wakati wa kubainisha mikakati ya utetezi, kujenga miungano, kuandaa jamii za wasiojiweza na kueleza wadau wakuu kuwa hatua za kufungwa kwa huduma ya intaneti si muhimu wala hazifai.

Tanzania pia ni moja ya nchi duniani ambapo matumizi ya mitandao ya VPN na zana za kukwepa udhibiti yamepigwa marufuku. The Electronic and Postal Communications Act prohibits the "use or distribution of tools that allow people to access prohibited content." Katika muktadha wa matukio ya kufungwa kwa huduma ya intaneti, hasa yanayolenga mifumo ya vyombo vya habari, mitandao ya VPN na zana nyingine za kukwepa udhibiti ni muhimu katika kuendelea kuwa mtandaoni na hata hivyo zinatumiwa na watumiaji wengi wa huduma ya intaneti nchini Tanzania. Kama inavyojadiliwa katika ripoti kamili, hofu na mashaka kuhusiana na uhalali wa matumizi ya mitandao ya VPN yanakanganya juhudi za harakati za utetezi.

Utafiti huu unalenga kutoa uchunguzi wa kina wa jinsi asasi za kiraia zinavyokadiria uwezekano na jinsi zinavyopanga kukabiliana na uwezekano wa kufungwa kwa huduma ya intaneti. Ripoti kamili (inayopatikana mtandaoni) inabainisha jinsi asasi za kiraia zinavyochukulia vitisho vya kufungwa kwa huduma ya intaneti nchini Tanzania na jinsi zinavyoelewa mbinu za kisheria na za kiufundi za hatua hizo za kufungwa kwa huduma, athari kwa jamii na uchumi iliyosababishwa na tukio la kufungwa kwa huduma ya intaneti mwaka wa 2020 kwa jamii muhimu, sheria na kanuni muhimu zinazowezesha kufungwa kwa huduma nchini, na nyenzo zinazohitajika ili kujiandaa na kupinga matukio ya kufungwa kwa huduma siku zijazo.

## Matokeo Muhimu Kutokana na Ukadiriaji wa Mahitaji ya Kufungwa kwa Huduma ya Intaneti Nchini Tanzania

- **Kuna ufahamu wa kiwango cha juu kuhusu matukio ya kufungwa kwa huduma ya intaneti, lakini kuna maarifa ya kiwango cha chini**. Licha ya kushuhudia hivi karibuni tukio la kufungwa kwa huduma yote ya intaneti katika kipindi cha uchaguzi wa urais wa mwaka wa 2020, bado kuna kiwango cha chini cha uelewaji kuhusu matukio ya kufungwa kwa huduma ya intaneti, hata kati ya waandishi wa habari na makundi ya asasi za kiraia.

- **Matukio ya kufungwa kwa huduma ya intaneti yana athari kubwa kwa demokrasia na uchumi**. Idadi kubwa (74%) ya wahojiwa walisema kuwa biashara zinazotegemea huduma ya intaneti huathiriwa zaidi na matukio ya kufungwa kwa huduma ya intaneti. Walipoulizwa hasa kuhusu jinsi matukio ya kufungwa kwa huduma ya intaneti yanavyoathiri maisha yao ya kila siku, idadi kubwa (74%) ya wahojiwa pia walisema kuwa matukio ya kufungwa kwa huduma ya intaneti yaliwazuia kufanya kazi zao na karibu nusu yao (48%) walisema moja kwa moja kuwa matukio ya kufungwa kwa huduma ya intaneti yaliwazuia kufanya biashara na kutengeneza pesa mtandaoni. Idadi kubwa (67%) ya wahojiwa pia walisema kuwa matukio ya kufungwa kwa huduma ya intaneti yaliathiri kibinafsi uwezo wao wa kupokea maelezo na habari muhimu, na idadi ya ziada ya 20%

ya wahojiwa walisema kuwa walizuiwa hasa kufanya kazi ya kampeni au kushiriki katika harakati za moja kwa moja za uhamasishaji.

- **Watu wana shaka sana kuhusu uwezekano wa matukio ya kufungwa kwa huduma ya intaneti siku zijazo kutokana na mabadiliko katika uongozi wa kisiasa.** Kwa sababu tukio la kufungwa kwa huduma ya intaneti la mwaka wa 2020 lilitokea kuhusiana na uchaguzi chini ya hayati Rais Magufuli, wahojiwa na washiriki katika mazungumzo ya kundi lengwa walitofautiana kuhusu uwezekano wa tukio la kufungwa kwa huduma ya intaneti siku zijazo. Karibu nusu (49%) ya wahojiwa katika utafiti walisema kuwa hawajui au hawana uhakika iwapo Tanzania itashuhudia tukio la kufungwa kwa huduma ya intaneti katika kipindi cha miaka mitatu ijayo. Karibu idadi sawa ya wahojiwa walisema kuwa inawezekana au inawezekana sana (20%) ikilinganishwa na waliosema kuwa haiwezekani au haiwezekani sana (19%) kuwa tukio la kufungwa kwa huduma ya intaneti litatokea nchini Tanzania katika kipindi cha miaka mitatu ijayo. Washiriki katika mazungumzo ya kundi lengwa walisisitiza kuwa shaka hii inatokana zaidi na kutofahamu hatua zitakazochukuliwa na Rais Hassan na serikali yake kuhusiana na uchaguzi ujao wa urais wa mwaka wa 2025.

- **Harakati za utetezi bado zinadhibitiwa na mikakati ya kisheria si wazi**. Kuna shaka kubwa, hata kati ya wataalamu wa kisheria, kuhusu sheria zinazoruhusu hatua za kufungwa kwa huduma ya intaneti. Idadi kubwa (65%) ya wahojiwa walisema kuwa sheria nchini Tanzania zinafanya iwe rahisi kwa serikali kufunga huduma ya intaneti na kudhibiti habari za mtandaoni. Washiriki walizungumzia Sheria ya Mawasiliano ya Kielektroniki na Posta ya 2020 (Electronic and Postal Communications Act (2020)) na Sheria ya Uhalifu wa Mtandaoni ya 2015 (Cybercrimes Act (2015)) kama mifumo ya kisheria inayoruhusu kudhibitiwa kwa vyombo vya habari na mifumo ya mtandaoni kwa kiwango kikubwa. Washiriki wa mazungumzo ya kundi lengwa pia walitaja sheria mahususi zilizopitishwa au kurekebishwa katika miaka kadhaa iliyopita ambazo zinadhibiti uwezo wa asasi za kiraia kufanya kazi na kushiriki katika aina hii ya harakati za utetezi, ambazo ni Sheria ya Mashirika Yasiyo ya Serikali (Non-Governmental Organizations (NGO) Act) na Sheria ya Takwimu (Statistics Act).

- **Wadau wakuu hawana uwezo wa kutarajia, kujiandaa na kuzuia matukio ya kufungwa kwa huduma ya intaneti**. Idadi kubwa (69%) ya wahojiwa walisema kuwa asasi za kiraia zina uwezo mdogo au hazina uwezo wa kukomesha tukio lililopo la kufungwa kwa huduma ya intaneti linaloweza kutokea siku zijazo, na karibu nusu (52%) ya wahojiwa walikadiria kuwa asasi za kiraia zina uwezo mdogo au hazina uwezo wa kushiriki katika harakati za utetezi wa uzuiaji kuhusu matukio ya kufungwa kwa huduma ya intaneti. Washiriki wa mazungumzo ya kundi lengwa walisema kuwa kuna haja ya mafunzo, usaidizi na nyenzo za ziada kutolewa katika sehemu mbalimbali, ikijumuisha kuzidisha kiwango cha uhamasishaji wa umma kuhusu matukio ya kufungwa kwa huduma ya intaneti, na kukusanya habari sahihi na maalum kuhusu mitandao ya VPN na zana za kukwepa udhibiti, kutumia mbinu za kimkakati za kuwasilisha kesi mahakamani na mikakiti mingine ya harakati za utetezi, kupata maarifa na ujuzi wa moja kwa moja katika

kukusanya na kuchanganua data ya kiufundi ya mtandao na kuitumia katika harakati za utetezi na kuripoti, na kuboresha ujuzi wa kuripoti athari kwa jamii na uchumi.

- **Zana za kukwepa udhibiti zinatumika kwa wingi, lakini bado kuna shaka na hofu kuhusu matumizi ya zana hizi**. Kuna haja ya kuelewa zaidi kuhusu mitazamo na hofu za watu kuhusu hali ya uhalali wa mitandao ya VPN na zana zingine za kukwepa udhibiti wa kufungwa kwa huduma ya intaneti. Asasi za kiraia nchini Tanzania zina kiwango cha juu kiasi cha ufahamu kuhusu mitandao ya VPN na zana za kukwepa udhibiti, na nyingi huripoti kwa kutumia zana hizi. Idadi kubwa (71%) ya wahojiwa walisema kuwa wanafahamu zana hizi na wamewahi kuzitumia. Hata hivyo, walisema pia kuwa wana ufahamu mdogo -- na wasiwasi kwa kiwango fulani -- kuhusu masuala kama vile manufaa na mapungufu ya zana mbalimbali na uhalali wa kuzitumia. Pia, zana za kawaida zaidi zilizoripotiwa kuwa zinatumiwa na wahojiwa zilikuwa zile zinazopatikana kwa lugha za kigeni, ikijumuisha kivinjari cha Psiphon na ToR, pamoja na mitandao ya VPN inayolipiwa inayotangazwa zaidi. Licha ya viwango vya juu kiasi vya matumizi ya mitandao ya VPN nchini Tanzania, karibu nusu (48%) ya wahojiwa walisema kuwa walikuwa na wasiwasi/hofu kuhusu matumizi ya mitandao ya VPN na zana za kukwepa udhibiti. Washiriki wa mazungumzo ya kundi lengwa walizungumzia hofu yao kuhusu kutoeleweka kwa sheria za matumizi ya zana za kukwepa udhibiti.

- **Idadi ndogo ya watetezi wa asasi za kiraia wana maarifa ya kiufundi kuhusu vipimo vya mtandao ili kuripoti matukio ya kufungwa kwa huduma ya intaneti na athari yake**. Zaidi ya nusu (56%) ya wahojiwa walisema kuwa asasi za kiraia nchini Tanzanian zina uwezo mdogo au hazina uwezo wa kurekodi vipimo vya mtandao. Pia, kama sehemu ya utafiti wa maelezo ya msingi, ukosefu wa juhudi thabiti za kupima utendaji wa mtandao ulidhihirishwa kwa ukosefu wa data inayoonyesha wakati kamili wa kurudishwa kwa huduma ya intaneti kwenye mifumo mbalimbali, ukosefu wa data uliothibitishwa na mashirika makuu ya kurekodi vipimo vya mtandao. Harakati za utetezi kuhusu matukio ya kufungwa kwa huduma ya intaneti zinahitaji kuwa na ushahidi thabiti -- ndio maana kuna haja ya kuwafunza watu wengi jinsi ya kukusanya na kuchanganua vipimo hivyo. Washiriki wa mazungumzo ya kundi lengwa walisema kuwa wataalamu wa vyombo vya habari wanahitaji hasa maarifa haya ili kuripoti uwezekano wa matukio ya kufungwa kwa huduma ya intaneti siku zijazo ipasavyo na kwa njia ya wazi zaidi.

## Jiandae, Zuia, Pinga Bangladeshi: Mapendekezo ya Kuunga Mkono Harakati za Utetezi Dhidi ya Matukio ya Kufungwa kwa Huduma ya Intaneti

Katika warsha zilizopangwa kwa ajili ya mtandao wa Jiandae na Uzuie wa Tanzania, washiriki wa warsha waliombwa kutafakari kuhusu matokeo ya utafiti na kubainisha malengo na shabaha za kujaza mapungufu ya ujuzi yaliyopo na kuanzisha mitandao ya harakati za utetezi yenye uwezo wa kujiandaa, kuzuia na kushughulikia matukio ya kufungwa kwa huduma ya intaneti. Malengo haya yanajumuisha:

- **Kutoa mafunzo kwa wadau wakuu ili waweze kutarajia, kujiandaa na kuzuia vyema matukio ya kufungwa kwa huduma ya intaneti**. Hii inamaanisha mafunzo, usaidizi na nyenzo za ziada kuhusu mada mbalimbali zinahitajika, ikijumuisha kuzidisha kiwango cha uhamasishaji wa umma kuhusu matukio ya kufungwa kwa huduma ya intaneti, kukusanya na kuchanganua habari sahihi na maalum kuhusu mitandao ya VPN na zana za kukwepa udhibiti, kuweka mkakati wa kuwasilisha kesi mahakamani na mikakati mingine ya harakati za utetezi inayoweza kutumika, kukuza maarifa na ujuzi wa moja kwa moja katika kukusanya na kuchanganua data ya kiufundi ya mtandao na kuitumia katika harakati za utetezi na kuripoti, na kukuza ujuzi na ufadhili wa kuripoti athari ya matukio ya kufungwa kwa huduma ya intaneti.

- **Kushiriki katika utafiti ili kuelewa vizuri mitazamo na hofu za watu kuhusu matumizi ya mitandao ya VPN na zana nyingine za kukwepa udhibiti wa kufungwa kwa huduma ya intaneti**. Hii inapaswa kujumuisha kufanya utafiti kuhusu matumizi ya sasa ya mitandao ya VPN kati ya makundi muhimu kama vile waandishi wa habari, vijana na jamii za wasiojiweza. Kisha matokeo ya utafiti huu yanapaswa kutumiwa kutoa miongozi maalum zaidi kuhusu jinsi ya kutumia zana hizi katika matukio tofauti ya kufungwa kwa huduma ya intaneti.

- **Kuunga mkono asasi za kiraia katika kuunda miungano ya wadau wengi kwa kufikia washirika wasio wa kawaida kama vile watoa huduma za intaneti (ISP), sekta za uchumi, taasisi za elimu na watoa huduma za afya**. Kuna haja ya kushirikisha mawakili, waandishi wa habari na wanateknolojia (kama vile wasanidi programu, wahandisi wa mtandao, nk.) katika harakati hizi za utetezi, ili kutumia uwezo wao tofauti katika kukabiliana na matukio ya kufungwa kwa huduma ya intaneti. Kwa mfano, watoa huduma za intaneti (ISP), hupata hasara kubwa za kifedha katika matukio ya kufungwa kwa huduma ya intaneti, wana uwezo mkubwa wa kupinga amri za serikali za kufungwa kwa huduma ya intaneti, wanaweza kutoa habari ili kufanya utaratibu wa kufungwa kwa huduma ya intaneti kuwa wa uwazi zaidi, na wana ufahamu kuhusu athari za kiuchumi za kufungwa kwa huduma ya intaneti kwa wateja wao. Habari hizo zinaweza kuwa muhimu kwa juhudi za kuelimisha umma kupitia vyombo vya habari na kwa mawakili kuzitumia kama ushahidi katika harakati zao za utetezi au kuwasilisha kesi mahakamani, ikiwa inahitajika.

- **Kuwafunza waandishi wa habari, Mashirika ya Asasi za Kiraia (CSO) na wanaharakati kuhusu jinsi ya kukusanya na kuchanganua data ya vipimo vya mtandao ya kutumiwa katika kuelimisha umma na katika harakati za utetezi**. Kuna haja ya kuhakikisha kuwa vipimo vinakusanywa mara kwa mara, na hasa kabla, wakati na baada ya matukio ya udhibiti kutokea.

- **Kutoa ufadhili na mafunzo kwa Mashirika ya Asasi za Kiraia (CSO) kuhusu zana za usalama wa mtandaoni na mbinu ambazo vinginevyo hayawezi kuzipata**. Hatua hii itayasaidia kujiandaa vizuri ili kukabiliana na kupunguza athari ya matukio ya kufungwa kwa huduma ya intaneti. Zana zinapaswa kujumuisha mitandao ya VPN, SIM kadi za kimataifa na nyenzo za kuelimisha kuhusu njia mbadala za kuwasiliana katika kipindi cha kufungwa kwa huduma ya intaneti.

- **Kutoa msaada kwa makundi ya wasiojiweza kama vile wanawake, vijana na walemavu, ambao mara nyingi huathiriwa kwa kiwango kikubwa na matukio ya kufungwa kwa huduma ya intaneti**. Makundi haya lazima yawezeshwe kuelewa matukio ya kufungwa kwa huduma ya intaneti, zana za kukwepa udhibiti wanazoweza kutumia ikiwa programu zimezuiwa, na nyenzo ambazo ni muhimu kwa lugha na viwango mbalimbali vya elimu.

- **Kukuza utaalamu wa kisheria na mbinu za kimkakati za harakati za utetezi**. Wataalamu wa kisheria wanahitaji ufahamu zaidi kuhusu matukio ya kufungwa kwa huduma ya intaneti na kuelewa vizuri zaidi manufaa ya kuwasilisha kesi mahakama dhidi ya taasisi za serikali zinazohusika na matukio ya kufungwa kwa huduma ya intaneti kimakusudi. Zaidi ya hayo, wataalamu hawa wanahitaji mafunzo kuhusu jinsi ya kushirikiana na makundi yanayokusanya na kuchanganua data ya mtandao, ili kujumuisha ushahidi kwenye kesi hizo. Idara ya mahakama inapaswa pia kuhamasishwa kuhusu masuala haya kwa sababu mahakimu katika nchi nyingine kama vile Zambia katika kipindi cha nyuma waliwahukumu watoa huduma kuhusu matukio ya kufungwa kwa huduma ya intaneti kutokana na amri ya serikali.

- **Kuwasaidia mawakili na watafiti kuelewa vizuri Sheria ya Mawasiliano ya Kielektroniki na Posta (Electronic and Postal Communications Act).** Hii itawasaidia kuelewa vizuri jinsi ya kutarajia uwezekano, kupigania kuwekwa kwa sheria zisizokanganya na zenye udhibiti mdogo, na kubuni mbinu za kimkakati za kuwasilisha kesi mahakamani ikiwa inahitajika. Juhudi za ziada zinapaswa kufanywa ili kuelewa jinsi sheria zingine (kama vile sheria ya usajili wa Mashirika Yasiyo ya Serikali (NGO)) zinavyoathiri mazingira ya utendakazi wa asasi za kiraia na uwezo wa miungano wa kushiriki katika harakati za utetezi kuhusu matukio ya kufungwa kwa huduma ya intaneti. Inaweza pia kusababisha fursa za kimkakati zinazoweza kujitokeza za kurekebisha sheria hizi katika kipindi cha urais wa Hassan.

- **Kuhakikisha msaada wa kifedha kwa gharama za kuweka mkakati wa kuwasilisha kesi mahakamani**. Hiyo inapaswa kujumuisha ununuzi wa zana za usalama wa mtandaoni kwa wataalamu wa kisheria.

Mapendekezo haya kwa sasa yanatekelezwa kupitia mradi wa OPTIMA wa shirika la Internews na Mtandao wa Jiandae, Zuia, Pinga nchini India, unaoongozwa na shirika la Change Tanzania na Internet Society Tanzania. Tunahimiza watu wanaovutia kushiriki wawasiliane na waandishi ili kushiriki katika shughuli za muungano na kuunga mkono kazi hii.

Tafadhali wasiliana nasi (lhenderson@internews.org, whitehead@internews.org) kwa maelezo zaidi kuhusu ripoti hii na ripoti nyingine za mahitaji ya harakati za utetezi kuhusu tukio la kufungwa kwa huduma ya intaneti za OPTIMA, mbinu yetu, na mitandao na nyenzo zetu za Jiandae na Uzuie.